

MSHANGILIENI MUNGU

14e Dim. T.O.C

Musique: Charles NYENZE

Texte: Zaburi 65

$\text{♩} = 70$

Mshangi-li-e-ni Mu - ngu e - nyi nchizo - te. (zo - te) nyi nchizo -

6
te

1. Mshangilieni Mungu, enyi nchi zote
 Uimbieni utukufu wa jina lake, mtoleeni sifa tukufu
 Mwambieni Mungu:
 Matendo yako jinsi yaliyo ya kutisha.

2. Dunia nzima ikusifu na kukuimbia,
 ilimbe jina lako,
 Njooni , tangazeni matendo ya Mungu:
 amefanya ya kutisha kati ya wanadamu.

3. Aligeuza bahari kuwa nchi kavu: watu walivuka mto kwa miguu
 Kwa hiyo twataka kumfurahia.
 Atawala kwa ezi yake ya milele,
 macho yake yawaangalia mataifa.

4. Njooni , sikieni wote wanaomheshimu Mungu,
 Nitawaelezea makuu alionitendea roho yangu
 asifiwe Mungu: hakunyima maombi yangu,
 wala hakuhepusha nami wema wake.